24 Septemba 2018

Mashirikisho ya Korea Kaskazini
na Ukiukaji wa Vikwazo Barani Afrika
Imetayarishwa na Kathrin Kranz, PhD

1. UTANGULIZI

Mashirikisho ni mashirika makubwa yanayoundwa kwa kuunganisha kampuni anuwai ambazo ziko mbalimbali.[1] Mashirikisho ya Korea Kaskazini yamepangwa na kufadhiliwa vizuri na yana sifa ya ongezeko la uhodari kwenye mbinu zao za kukiuka vikwazo. Kwa hakika, ripoti ya hivi karibuni ya Jopo la Wataalamu la Umoja wa Mataifa imebaini kwa masikitiko kuwa Korea Kaskazini "inaendelea kuenda kinyume na marufuku ya silaha na vikwazo vikali vya kifedha na kinyanja, na inaonyesha kuwa kila ukali wa vikwazo unavyopanuka, uwezo wa ukiukaji pia unapanuka."[2] Kuna uwezekano mkubwa kuwa shughuli hizi za kuvunja vikwazo zitaendelea. Ukweli ni kuwa vikwazo vya kina zaidi dhidi ya Korea Kaskazini vinaweza kuimarisha nguvu na ushawishi wa mashirikisho.[3] Kwa hivyo, ni muhimu sana kuelewa mikakati inayotumiwa na mashirikisho ya Korea Kaskazini ili kukwepa vikwazo. Mikakati hii inajumuisha matumizi ya lakabu ya watu na kampuni za Korea Kaskazini, kuhusisha wanadiplomasia, wafanyikazi wa ubalozi na balozi, mipango ya safari yanayofanywa kwenye nchi ambazo mipango hiyo inaweza kufichika kwa urahisi zaidi, modeli za mashirika yaliyojitenganisha, na kuingiza kampuni za Korea Kaskazini kwenye kampuni za nchi zingine. Uelewaji bora zaidi wa mikakati utarahisisha kuangamiza ukwepaji wa vikwazo, na pia utazuia gharama za sifa zinazohimiliwa na serikali ambazo zinachukuliwa kuwa zinahusika kwenye ukiukaji wa vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini.

2. MASHIRIKISHO YA KOREA KASKAZINI

Mashirikisho ya Korea Kaskazini yanafafanuliwa vizuri kabisa kama "ushirikiano baina ya serikali na kampuni binafsi."[4] Kulingana na sheria za Korea Kaskazini, serikali ni mhusika wa kipekee kwenye uchumi na inamiliki kampuni zote. Ijapokuwa kampuni zinaendeshwa na watu binafsi, na pia zinategemea kiasi ufadhili binafsi wa waheshimiwa matajiri wa Korea Kaskazini[5], uhusiano na serikali ni muhimu uzingatiwe kwa ajili uhusiano huu unashawishi mfululizo wa mbinu zipatikanazo zinazotumiwa na Korea Kaskazini na mashirikisho yake ili kukiuka vikwazo, kama ilivyoelezwa ndani ya kifungu cha tatu na cha nne cha ripoti hii.

Pia ni muhimu kuzingatia kuwa tangu mwaka wa 2014, mameneja wa kampuni zinazomilikiwa na serikali nchini Korea Kaskazini wameruhusiwa kufanya biashara na kuunda

Rico Carisch
rico.carisch@comcapint.com
+1-610-390-9541

www.comcapint.com
110 West 94 Street – 2D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
loraine.rickard-martin@comcapint.com
+1-917-715-2142

miradi ya pamoja na raia wa kigeni.[6] Hii inaleta utata zaidi wa kugundua na kutathmini shughuli za mashirikisho ya Korea Kaskazini, na inaangaziwa kwenye mtandao wa kimataifa na mashirika yanayoendeshwa na raia wa kigeni yanayoshirikiana na mashirikisho haya. Mikakati ya kuenda kinyume na vikwazo, kama vile kuingiza kampuni za Korea Kaskazini kwenye mashirika ya nchi zingine, ni lazima yaangaziwe ndani ya muktadha huu.

Kwa ziada, kwa ajili vikwazo vya kina zaidi vinazidi kuzitilia shinikizo kampuni za Korea Kaskazini, ushawishi na nguvu za mashirikisho zinatarajiwa kuongezeka. Kama vile wataalamu walivyotabiri, hali ni hii kwa sababu kampuni ndogo na za wastani hazina uwezo unaohitajika kukwepa vikwazo.[7] Kwa ajili ya haya, shughuli za kampuni ndogo na za wastani zinadhibitiwa sana. Pia, biashara na shughuli za kibiashara za Korea Kaskazini zinaweza kusisitiza zaidi mashirikisho, na kuongeza umuhimu wa mashirikisho kwenye uchumi wa Korea Kaskazini. Kutokana na haya, Korea Kaskazini itaongeza juhudi zake za kukiuka vikwazo ili kulinda mashirika yake yanayoiletea pesa yaliyoko ng'ambo.

Mashirikisho ambayo ni muhimu kabisa yaangaziwe ili kuelewa shughuli za Korea Kaskazini barani Afrika (na kwingine) zinatangulizwa hapo chini.

2.1 Shirika Husiani la Green Pine (Green Pine)/Shirika la Biashara la Korea la Kuendeleza Uchimbaji Madini (KOMID)

Shirika Husiani la Green Pine (Green Pine) lilichukua nafasi ya Shirika la Biashara la Korea la Kuendeleza Uchimbaji Madini (KOMID) baada ya KOMID kuorodheshwa mnamo 24 Aprili 2009. Green Pine ilifuata kwa kuorodheshwa mnamo 2 Mei 2012.[8] Green Pine /KOMID ni shirikisho kuu la kuuza silaha na kusafirisha hadi ng'ambo bidhaa na vifaa vinavyohusiana na makombora ifikayo mbali na silaha za kawaida.[9] Inafanya shughuli zake kwa kufuata amri za Shirika la Upelelezi wa Jumla, huduma kuu ya upelelezi wa nje ya Korea Kaskazini.[10]

Green Pine, na kabla yake, KOMID, zina kampuni kadhaa zinazohusika nazo, zinafanya shughuli zake huko ng'ambo kwa kutumia lakabu, na zinashirikiana na kampuni ambazo zinaweza kuwa au zinaweza zisiwe sehemu za moja kwa moja za mashirikisho yake. Kwa ajili ya utata wa mashirikisho ya Green Pine/KOMID na taratibu zao, ni muhimu kuzingatia baadhi ya mitandao yaliyoundwa na Green Pine/KOMID.

Kwa mfano, KOMID ilishirikiana na Kundi la Kampuni la Mradi wa Nje la Mansudae (Mansudae), kampuni ya ujenzi ya Korea Kaskazini. Mansudae imesimamia taratibu za ujenzi ndani ya angalau nchi 14 barani Afrika, "ikijenga kila kitu kama vile mitambo ya risasi, ikulu za marais, na majengo ya kuishi."[11] Hadi hivi karibuni, Mansudae ilikuwa na makao makuu nchini Namibia, ambapo Mkurugenzi Msimamizi wake alikuwa Kim Tong Chol (ambaye pia ni mwakilishi wa nje wa Benki ya Biashara za Nje).[12] Iliorodheshwa na Baraza la Usalama mnamo 5 Agosti 2017 kwa kushiriki kwenye, kusaidia, au kuhusika kwenye usafirishaji wa wafanyikazi kutoka Korea Kaskazini hadi mataifa mengine, yakiwemo Aljeria, Angola, Botswana, Benini,

Chadi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ginekweta, Msumbiji, Namibia, Togo na Zimbabwe.[13] Kwa pamoja, KOMID na Mansudae zilishutumiwa kwenye ujenzi wa kiwanda cha silaha nchini Namibia.

Shirika la kifedha la KOMID pia lilitegemea kampuni zingine, ambazo pia zilishutumiwa kwenye ukiukaji wa vikwazo. Benki ya Kibiashara ya Tanchon (iliyokuwa ikijulikana kama Benki ya Mkopo ya Changwang FKA: Benki ya Mkopo ya Korea Changwang) ndio tawi kuu la kifedha la KOMID.[14] Inahusishwa na kampuni kadhaa zilizoorodheshwa, zikiwemo Benki ya Maendeleo ya Amroggang na Shirika la Benki la Kwangson, ambazo pia zinafanya miamala ya kifedha kwa niaba ya KOMID.[15]

Green Pine, kwa upande mwingine, inafanya shughuli zake kwa kutumia lakabu kadhaa, kama vile Shirika la Uwekezaji na Maendeleo ya Rasilimali za Kiasili na Shirika la Uwekezaji au Shirika la General Precious Metal.[16] Benki ya East Land inarahisisha miamala ya silaha, au usaidizi mwingine kwa, Green Pine. Iliorodheshwa mnamo 29 Oktoba 2014 na "imefanya kazi na Green Pine ili kusafirisha fedha kwa njia inayokwepa vikwazo."[17] Rais wa Green Pine ni Ri Hak Chol, ambaye ameenda Angola, Misri, na Jamhuri ya Kiislamu ya Irani, licha ya kuwa vikwazo vilinuiwa kumzuia asifanye safari kama hizi.[18]

2.2 Benki ya Biashara za Nje

Benki ya Biashara za Nje ni benki inayomilikiwa na serikali inayofanya kazi kama benki kuu ya Korea Kaskazini ya kubadilisha sarafu za kigeni. Iliorodheshwa mnamo 5 Agosti 2017 kwa sababu ilitoa usaidizi wa kifedha kwa Shirika la Benki la Korea Kwangson (KKBC). KKBC iliongezwa kwenye Orodha ya Watu, Kampuni na Mashirika Mengine Yaliyotajwa mnamo 2 Machi 2016 kwa ajili ya kutoa huduma za kifedha kwa Benki ya Kibiashara ya Tanchon (tawi la kifedha la KOMID) na Shirika la Biashara la Korea Hyoksin, kampuni iliyoko chini ya amri ya Shirika la Jumla la Korea Ryonbong, iliyoshutumiwa kwa kusaidia mradi wa silaha za nyuklia za Korea Kaskazini.[19]

2.3 Kampuni ya Usimamizi ya Ocean Maritime

Kampuni ya Usimamizi ya Ocean Maritime, Ltd. (OMM) iliongezwa kwenye Orodha ya Watu, Kampuni na Mashirika mengine Yaliyotajwa mnamo 28 July 2014 kwa ajili ya kuhusika kwake kwenye usafirishaji wa mizigo iliyofichwa yenye silaha na bidhaa husika.[20] Kabla ya kuorodheshwa, OMM lilikuwa shirika kubwa kabisa la usafirishaji la Wizara ya Usafiri wa Ardhi na Bahari. OMM imeunda mtandao mpana wa ofisi barani Asia, Uropa, Amerika Kusini na Mashariki ya Kati. Inafanya shughuli zake kwa kutumia meli 35, ambazo usajili wake unabadilishwa mara kwa mara kwa ajili ya kuogopa vikwazo.[21]

3. UKIUKAJI WA KIMSINGI WA VIKWAZO BARANI AFRIKA

Ukiukaji kadhaa wa vikwazo unaweza kurekodiwa kulingana na ripoti za Umoja wa Mataifa na ripoti za vyombo vya habari. Kifungu hiki kinaorodhesha ukiukaji wa kimsingi uliofanywa na mashirikisho matatu makuu (kwa ajili ya utata wa mifano haya, shughuli za KOMID na Green Pine zinazungumziwa kando). Ni muhimu kuzingatia kuwa shughuli na wawakilishi wa mashirikisho anuwai mara nyingine yanaingiliana. Vikwazo anuwai vimekwepwa, vikiwemo miiko ya usafiri, na marufuku ya kifedha, silaha, ushirikiano wa kijeshi, na biashara.

3.1 KOMID/ Green Pine

3.1.1 KOMID

3.1.1.1 Namibia

KOMID ilitoa vifaa muhimu vya kujenga kiwanda cha silaha cha Oamites nchini Namibia kwa kushirikiana na, au kwa kutumia lakabu ya, kampuni za Kundi la Mradi wa Nje wa Mansudae.[22] Mansudae ilitumia wafanyikazi waliotoka nchini Korea Kaskazini. Namibia ilithibitisha kuwa Mansudae ilihusika kwenye miradi kadhaa ya ujenzi wa kijeshi, ikiwemo shule ya kijeshi na makao makuu ya Wizara ya Ulinzi, lakini ilikataa kuwa ilikuwa inajua kuhusu uhusiano baina ya Mansudae na KOMID.[23]

Kwa ziada, KOMID iliipatia Namibia aina anuwai za mashine na matangi ya shinikizo yanayoweza kutumiwa kwenye vilipuzi vya kijeshi na uzalishaji wa rafadha.[24]

Ubalozi wa Korea Kaskazini nchini Afrika Kusini ulisaidia maafisa wa KOMID ambao waliunda akaunti ya benki nchini Namibia kwa kutumia majina yao.[25]

3.1.1.2 Uganda

Imeripotiwa kuwa KOMID ilitoa mafunzo kwa jeshi na polisi nchini Uganda, na haswa jeshi la wanahewa la Uganda.[26] Shughuli hizi zilisaidiwa na mwananchi wa Korea Kaskazini aliyeorodheshwa, Ryu Jin. Alitumia Shirika la Biashara ya Teknolojia la Tosong na Benki ya Kibiashara ya Tanchon kama kampuni zilizomilikiwa ili kukwepa vikwazo dhidi yake. Inaaminiwa kuwa anasafiri kwa kutumia lakabu.

Pia imeripotiwa kuwa ofisi ya mwakilishi wa kijeshi kwenye Ubalozi wa Korea Kaskazini huko Kampala, Uganda, imejaribu kutoa huduma za kijeshi zisizoruhusiwa.[27]

3.1.1.3 Sudani

Maafisa wawili wa KOMID nchini Sudani ni Kim Song Chol, ambaye pia anatumia lakabu ya Kim Hak Song, na Song Jong Hyok, ambaye pia anatumia lakabu ya Son Min.[28] Maafisa wote wawili walifukuzwa nchini Misri, na, kulingana na ripoti zinazochunguzwa na Jopo la Wataalamu la Umoja wa Mataifa, walikuwa ndio msingi wa uhusiano baina ya Sudani na Korea Kaskazini. Inadaiwa kuwa KOMID inashirikiana na Shirika la Kiwanda la Kijeshi linalodhibitiwa na Serikali ya Sudani. Kwa ziada, mizigo inayopelekwa kupitia ndege au meli kutoka Korea Kaskazini hadi Sudani inayohusiana na KOMID inachunguzwa.[29]

Korea Kaskazini pia ilisafirisha sehemu mia za udhibiti za roketi zinazoongozwa kwa usahihi za milimita 122 na makombora themanini ya kuvamia hewani yanayoongozwa kwa satalaiti hadi kwa Kampuni Kuu ya Uhandisi wa Teknolojia nchini Sudani. Mikataba ya mauzo yalitiwa saini na rais wa KOMID, Kang Myong Chol (mwenye lakabu ya Pak Han Se), kwa kutumia kampuni ifichayo KOMID, Kampuni ya Biashara ya Teknolojia ya Chosun Keunchon.[30] Kim Song Chol, aliyekuwepo nchini Misri wakati huo, alienda Khartoum kama sehemu ya makubaliano, na aliandamana na wafanyikazi 13 wa KOMID.[31]

Kulingana na toleo la wanahabari wa Idara ya Fedha nchini Marekani, mwakilishi wa KOMID, Jang Song Chol, “anafanya kazi na watu walioko nchini Sudani ambao wanapata bidhaa kutoka kwake,” ambayo inazidi kudokeza kuwa kuna makubaliano ya kijeshi baina ya Sudani na Korea Kaskazini.[32]

3.1.2 Green Pine

3.1.2.1 Angola

Jopo la Wataalamu la Umoja wa Mataifa lilichunguza wanadiplomasia wa Korea Kaskazini waliothibitishwa nchini Angola wanaofanya kazi kwa niaba ya Green Pine ambao washawahi kushiriki kwenye shughuli zisizoruhusiwa zinazohusiana na silaha.[33]

Jopo pia linaendelea uchunguzi wake wa mafunzo ya walinzi wa rais wa Angola yaliyotolewa na wafanyikazi wa Korea Kaskazini na wanadiplomasia waliothibitishwa nchini Angola wanaofanya kazi kwa niaba ya Green Pine. Mwanadiplomasia mmoja, Kim Hyok Chan, alikuwa na jukumu la kuunda upya meli za kijeshi za wanamaji wa Angola ambayo inakiuka vikwazo.[34] Yeye, pamoja na mwakilishi wa Green Pine, Jon Chol Young, walisafiri hadi Sri Lanka mara tatu ili kuzungumzia miradi ya kujenga meli.

Angola iliripoti kuwa Green Pine ilikuwa ikiwapatia boti za kijeshi za kushika doria hadi mwaka wa 2012. Rekodi za ushuru za Uchina pia zinaonyesha kuwa kampuni ambayo ina makao yake makuu mjini Beijing inayohusishwa na Green Pine iliiuzia Angola bidhaa zenye matumizi mawili zinazohusiana na usafiri baharini, zikiwemo injini za boti, mota, na mifumo ya rada.[35]

Kwenye miezi ya Februari na Julai 2011, mwananchi wa Austria, Josef Schwartz, alisaidia Green Pine kusafirisha vifaa vya boti za kijeshi za kushika doria na sehemu za nyambizi hadi Angola.[36]

3.1.2.2 Misri

Shirika la Biashara la Saeng Pil, lakabu ya Green Pine, lina shughuli nyingi huko Kairo. Mwanadiplomasia wa Korea Kaskazini, An Jong Hyuk, aliteuliwa awe mwakilishi wa Shirika hilo, na mnamo 18 Disemba 2013, alipewa idhini ya kufanya biashara za kila aina, zikiwemo kutekeleza mikataba na biashara za benki.[37]

3.1.2.3 Eritrea

Jopo la Wataalamu lilithibitisha uhusiano na jeshi baina ya Green Pine na Idara ya Magereji ya Serikali (ambayo ina jukumu la kudumisha na kuunda upya mifumo ya silaha).[38]

3.1.2.4 Msumbiji

Jopo la Wataalamu lilipokea maelezo kuhusu safari za kuenda na kutoka Msumbiji baina ya miaka ya 2012 na 2017 zilizofanywa na wananchi watano wa Korea Kaskazini wanaofanya kazi kwa niaba ya KOMID na Green Pine ambao wamehusishwa na biashara ya silaha za kawaida na ulanguzi wa silaha kwenye nchi nyingine barani Afrika.[39]

3.1.2.5 Zimbabwe

Jopo la Wataalamu linachunguza shughuli za wananchi wa Korea Kaskazini nchini Zimbabwe, ambao wamehusishwa kwenye biashara ya silaha barani Afrika na Mashariki ya Kati.[40]

3.2 Benki ya Biashara za Nje

3.2.1 Tunisia

Wawakilishi wa Benki ya Biashara za Nje walitumia jina la kampuni ifichayo, “Kartos”, ili kufungua akaunti kwenye Benki ya Kiarabu ya Tunisia.[41] Mwakilishi mmoja wa Biashara za Nje ambaye yuko ng’ambo, Ri Chun Song, alikuwa na idhini ya kutia saini ya akaunti ya dola za Marekani na akaunti ya Yuro kwenye banki hiyo hiyo. Akaunti ya Yuro ilifunguliwa na Chun Song aliyejitambulisha kama “Mjumbe wa Katibu wa Ziara ya Korea Kaskazini huko Tripoli.” Tangu hapo, akaunti zote mbili zimefungwa.

3.2.2 Libya

Mwakilishi mkuu wa Benki ya Biashara za Nje nchini Libya, , Ku Ja Hyong, ameshutumiwa kwa ajili ya kusafiri hadi Tunisia, Muungano wa Falme za Kiarabu, na Saudi Arabia, baina ya 2015 na 2017, na kwa ajili ya kusafiri na pasipoti mbili.[42] Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ya 2321 (2016) na 2270 (2016) yanayozilazimu nchi ambazo ni wanachama zimtoe mtu yoyote ambaye anajulikana kuwa anafanya kazi kwa niaba ya au kwa kulekezwa na benki ya Korea Kaskazini.

3.3 Kampuni ya Usimamizi ya Ocean Maritime (OMM)

3.3.1 Misri

Wawakilishi wa OMM walikuwa wamejiingiza ndani ya wakala wa Sunlight, yanye makao makuu yake mjini Port Said, hadi 2011. Walitumia mada za "Ocean Egypt" na "Ocean Maritime Management Egypt," ingawa OMM haikuwahi kusajiliwa rasmi nchini Misri. Wawakilishi wa OMM, wakiwemo wananchi wa Korea Kaskazini, walitoa usaidizi wa mipango ya usafiri na usaidizi wa kitaratibu kwa meli za OMM, kama vile kuwacha meli zao zipite kwenye Mfereji wa Suez.

Wakala ya Sunlight pia ilifanya kazi kama anwani ya "Tonghae P(ort) Said", ambayo inaonekana kuwa ni ofisi ya tawi ya kampuni zinazohusiana na OMM, Korea Tonghae au Tonghae Sonbak. Korea Tonghae pia ilikuwa na ofisi ndani ya Ubalozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea huko Kairo.[43]

4. CHANGAMOTO ZA KUTAMBUA NA KUZUIA UKIUKAJI WA VIKWAZO VILIVYOWEKEWA KOREA KASKAZINI

Mifano ya ukiukaji wa vikwazo inayoelezwa ndani ya kifungu cha tatu inatoa fursa ya kutambua mikakati kadhaa ambayo imetumiwa na Korea Kaskazini—na ambayo inaendelea kutumiwa na Korea Kaskazini—ili kukwepa vikwazo.

4.1 Lakabu

Wawakilishi wa Korea Kaskazini mara nyingi wanatumia lakabu ili kuficha utambulisho wao na kukwepa vikwazo vinavyowazuia wasiweze kusafiri nje. Kwa mfano, Ko Tae Hun, mwakilishi wa nje wa Benki ya Kibiashara ya Tanchon nchini Sudani, amekuwa kwenye Orodha ya Watu, Kampuni na Mashirika mengine Yaliyotajwa tangu 2 Machi 2016.[44] Ameenda Uchina, Uhabeshi na Muungano wa Falme za Kiarabu kwa kutumia lakabu ya "Kim Myong Gi".[45]

Vivyo hivyo, mashirikisho yanatumia lakabu ili kuyapatia fursa ya kuendelea kufanya shughuli huko ng'ambo bila kugunduliwa. Green Pine inafaa kuangaziwa kuhusiana na haya, kwani, kwa kutumia lakabu, imefungua ofisi kadhaa kwenye nchi za ng'ambo, zikiwemo Uchina.[46]

4.2 Wanadiplomasia, wawakilishi, na mabalozi

Wawakilishi wa mashirikisho wanafanya shughuli zao ndani ya balozi, wanashirikiana moja kwa moja na wanadiplomasia na wafanyikazi wa ubalozi, na wanathibitishwa wawe wanadiplomasia ili kurahisisha shughuli zao huko ng'ambo.

Kwa mfano, vyombo vya habari vimeripoti kuwa maafisa wa KOMID wanafanya kazi pamoja na balozi za Korea Kaskazini ili kukuza mauzo. Kulingana na gazeti la The New York Times, mwakilishi wa KOMID, Son Jong Hyok, amefanya kazi na Balozi Pak Chol Il wa Ubalozi wa Korea Kaskazini ulioko Kairo, Misri, ili kuuza silaha za Korea Kaskazini kwa nchi zilizoko barani Afrika.[47] Ubalozi wenyewe umefafanuliwa kuwa "unafanya kazi ya pili kama duka la silaha la kieneo" na "soko linalovuma la mauzo ya siri ya miundombinu ya kijeshi ya nyakati za Sovieti yaliyopunguzwa bei na makombora ya Korea Kaskazini yanayouzwa Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati."[48]

Jopo la Wataalamu pia limeona ruwaza ambapo Korea Kaskazini inawathibitisha wawakilishi wa ng'ambo wa Green Pine wawe wanadiplomasia.[49] Nchini Angola, kwa mfano, Kim Hyok Chan, mwanadiplomasia na mwakilishi wa Green Pine, alifanya mazungumzo ya mikataba, alipata vyanzo vya vipuri, na alisimamia utengenezaji upya wa boti za kushika doria za jeshi la wanamaji la Angola.[50] Mfano wa Kim Hyok Chan si wa kipekee. Kuna ushahidi kuwa mwanadiplomasia wa pili, Jol Chol Young, pia alifanya biashara kwa niaba ya Green Pine.[51]

4.3 Mipango ya safari

Ili kuficha safari zao na maeneo ya kuwasili, wawakilishi wa Korea Kaskazini wanapitia nchi kadhaa kwa mfano Uchina, Uhabeshi, Muungano wa Falme za Kiarabu, Urusi,[52] na wananunua tikiti za ndege kwenye nchi nyingine, zikiwemo Jamhuri ya Kiarabu ya Siria na Misri.[53] Maafisa na wawakilishi wa mashirikisho wanasifiri kwa kutumia pasipoti kadhaa, na kuufanya utekelezaji wa vikwazo—kulingana na nambari za pasipoti zilizojumuishwa kwenye orodha za vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa—uwe mgumu.[54]

4.4 Modeli ya mashirika yaliyojitenganisha

Modeli za mashirika yaliyojitenganisha zinafafanua mashirikisho ya Korea Kaskazini, na zinaruhusu uanzilishi wa mitandao inayosaidia kuzitenganisha kampuni binafsi na wanaofaidika nchini Korea Kaskazini na wananchi ambao si wa Korea Kaskazini wanaoshirikiana na kampuni za Korea Kaskazini kwenye nchi nyingine.[55] Kwa mfano, Mansudae, iliyozungumziwa hapo juu

kuhusiana na KOMID, ilikuwa kwenye orodha ya kampuni zaidi ya kumi zilizohusishwa kwenye uchunguzi wa Kundi la Kampuni za Malesia-Korea (MKP) unaofanywa na Jopo la Wataalamu la Umoja wa Mataifa.[56] Jopo liligundua shirikisho la kampuni zilizoorodheshwa zinazojumuisha Mansudae, MKP, Shirika la Jumla la Ukaguzi, OMM, na Shirika la Benki la Korea Kwangson.

4.5 Kampuni zifichazo na matawi yao

Pamoja na modeli ya mashirika yaliyojitenganisha, kampuni zifichazo zinatumiwa kuficha kuhusika kwa kampuni za Korea Kaskazini. Kwa mfano, tawi la Misri la KOMID lilianzishwa na usaidizi wa moja kwa moja wa Pak Chun II, Balozi wa Korea Kaskazini nchini Misri.[57] Vivyo hivyo, KOMID ilianzisha kampuni zifichazo nchini Uchina, kama vile Kampuni Mpya ya Biashara ya Teknolojia ya Beijing.[58]

4.6 Kuingiza kampuni ndani ya kampuni zingine ili kuficha utambulisho wa kampuni

OMM ina kampuni zenye shughuli ndani ya nchi kadhaa. Kampuni hizi mara nyingi hazisajiliwi kisheria. Badili yake, zinaingizwa ndani ya kampuni za nchi ili kuficha uhusiano na OMM.[59] Mikakati hii inasaidiwa na njia inayohusika ya kuhamisha wawakilishi baina ya kampuni na nchi, na kwa kuwapatia wawakilishi ngao ya hadhi ya kidiplomasia.

4.7 Nchi za kirafiki

Ukiukaji wa vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini unasaidiwa na serikali za kirafiki ambazo zinatoa usaidizi wa moja kwa moja au usaidizi wa kivingine, au zinapuuza, shughuli za Korea Kaskazini.

Kimahususi, Misri imeonekana kuwa ni rafiki wa karibu wa Korea Kaskazini, na haijaficha usaidizi inayoipatia Korea Kaskazini.[60] Maafisa wa KOMID pia wameshughulika ndani ya Shirikisho la Urusi,[61] na mwakilishi wa nje wa Benki ya Biashara za Nje, Kim Tong Chol, alikuwa mkaazi nchini Uchina (baada ya kuorodheshwa).[62]

4.7 Matumizi ya raia wa kigeni

Kuna mifano ambapo raia maalum wa kigeni walionekana wanasaidia Korea Kaskazini kukwepa vikwazo bila ya usaidizi wa nchi zao. Mfano mmoja wa kuzingatiwa ni ule wa mwananchi wa Austria, Josef Schwartz, ambaye kupitia kampuni yake, Schwartz Motorbootservice & Handel GmbH, alisafirisha vifaa vya boti za kijeshi za kushika doria hadi Angola.[63] Schwartz alikuwa amefanya biashara na Korea Kaskazini mara kadhaa, zikiwemo ukiukaji wa marufuku ya bidhaa za anasa.

5. MAPENDEKEZO

5.1 Zingatia kwa makini mipango na hati za usafiri

Kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 4.3, kuna matukio ambapo maafisa wa Korea Kaskazini wanasafiri kwa niaba ya mashirikisho wakiwa na zaidi ya pasipoti moja. Kwa hivyo, nambari za pasipoti zilizoorodheshwa kwenye orodha ya vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa zinaweza kuwa sizo zile ambazo afisa anasafiri nazo. Ni muhimu sana kuzingatia kwa makini hati za usafiri ili kutambua wananchi wa Korea Kaskazini ambao wamepigwa marufuku wasisafiri nje. Njia tata za usafiri (haswa kupitia nchi za kirafiki kama vile Siria na Uchina) zinaweza kutumiwa kama ishara ya kutambua watu waliopigwa marufuku wasisafiri nje.

5.2 Chunguza uhusiano na kampuni zingine

Mikakati ya mashirika yaliyojitenganisha, kampuni zifichazo na matawi, na kuingiza kampuni ndani ya mashirika ya nchi zingine, inasisitiza umuhimu wa kuchunguza uhusiano na kampuni zingine (hii ni kwa mujibu wa uwezo wa nchi inayozungumziwa). Kuzingatia kwa makini Orodha ya Umoja wa Mataifa ya Watu, Kampuni na Mashirika mengine Yaliyotajwa kunapendekezwa ili kutambua kama kuna uhusiano baina ya kampuni na shirika lililoorodheshwa.

5.3 Boresha kuripoti kuhusu utiifu wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Korea Kaskazini

Mikakati inayotumiwa na mashirikisho ili kukwepa vikwazo inategemea usiri na ulaghai. Labda mojawapo ya njia nzuri kabisa za kupunguza ufanisi wa mikakati hii ni kuongeza kiwango cha kuripoti kwa Umoja wa Mataifa kuhusu shughuli zinazoshukiwa za Korea Kaskazini. Uwazi uliokuzwa unatoa fursa kwa Umoja wa Mataifa kutoa maelezo bora zaidi kwa nchi anuwai ambazo ni wanachama, na unaweza kusaidia kutambua juhudi za kukiuka vikwazo za Korea Kaskazini.

5.3 Zingatia ukiukaji wa vikwazo vilivyowekewa nchi zilizoko barani Afrika

Mfano wa shughuli za KOMID nchini Sudani unasisitiza kuwa mashirikisho hayakiuki vikwazo vilivyowekewa Korea Kaskazini tu, bali pia vinachangia kupunguza nguvu za vikwazo vilivyowekewa nchi zilizoko barani Afrika (kwa Azimio la 1591, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limewekea marufuku ya silaha dhidi ya Sudani ambayo inalenga Darfur tu. KOMID kulipatia Shirika la Kiwanda la Kijeshi la Sudani silaha kunaweza kuwezesha ukiukaji wa Azimio la 1591). Shughuli zinazosababisha ukiukaji anuwai wa vikwazo zinatia tumbo joto kuhusu sifa ya kimataifa ya nchi. Kwa hivyo, kuelewa vikwazo anuwai ni muhimu sana.

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

5.4 Unda uainishaji wa vikwazo na ukiukaji

Kuhusu kidokezo kilichopita, taratibu moja ya shirikisho inaweza kukiuka vikwazo anuwai vilivyowekewa Korea Kaskazini na mashirika yao. Ili kuelewa vizuri zaidi shughuli tata za mashirikisho, ni muhimu kuzingatia vikwazo vyote husika, kuchambua shughuli zipi haziruhusiwi, na kuzingatia athari za ukiukaji wowote unaojaribiwa. Hii inaweza kuboresha uelewaji wa majukumu ya nchi yanayohusu vikwazo vya Umoja wa Mataifa, na pia, kusaidia kutambua juhudi za Korea Kaskazini za kujaribu kuenda kinyume na vikwazo hivyo.

Kuhusu Kathrin Kranz

	Kathrin Kranz ana Ph.D. ya Mafunzo ya Usalama na Sayansi ya Kisisasa kutoka kwa Chuo Kikuu cha Notre Dame, na LL.M. ya Sheria ya Kimataifa ya Umma kutoka kwa Shule ya Uchumi na Sayansi ya Kisiasa ya London. Utafiti wake unaangazia biashara ya kimataifa ya silaha, vikwazo vya kiuchumi, na taasisi za kimataifa.

[1] "shirikisho" *OED Mtandaoni*. Oxford University Press, Juni 2018.
[2] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. "Ripoti ya muhula wa kati ya Jopo la Wataalamu iliyoundwa kulingana na azimio la 1874 (2009)." 5 Septemba 2017. http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2017/742, Muhtasari
[3] Andra Abrahamian "Vikwazo na Utafutaji Soko nchini Korea Kaskazini: Mafunzo kutoka kwa Myanmari," Februari 28, 2018, https://www.38north.org/2018/02/aabrahamian022818/
[4] Mwanauchumi "Kuanzia Ndege hadi Makereli. Aina Mpya za Mashirikisho Zinasaidia Kuiimarisha Korea Kaskazini," Januari 25, 2018
[5] Ibid. Mwanauchumi, 2018
[6] Ibid. Mwanauchumi, 2018
[7] Ibid. Abrahamian, 2018
[8] Idara Zinazomilikiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Kongamano la Baraza la Usalama Lililoundwa kwa Kutii Azimio la 1718 (2006) "Shirika Husiani la Green Pine," 2 Mei 2012. https://www.un.org/sc/suborg/en/sanctions/1718/materials/summaries/entity/green-pine-associated-corporation
[9] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. "Orodha iliyoundwa na kudumishwa kwa kutii azimio la 1718 (2006) la Baraza la Usalama. 24 Mei 2016. https://scsanctions.un.org/fop/fop?xml=htdocs/resources/xml/en/consolidated.xml&xslt=htdocs /resources/xsl/en/dprk.xsl.
[10] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Ripoti ya mwisho ya Jopo la Wataalamu iliyowasilishwa kwa kutii azimio la 1985 (2011), 14 Juni 2012. http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2012/422, Nyongeza ya X
[11] Hugh Griffiths amenukuliwa kwenye "Masanamu na risasi: Uhusiano wa Korea Kaskazini na Afrika," ya David McKenzie na Brent Swails *CNN*, 15 Disemba 2017. https://edition.cnn.com/2017/10/22/africa/north-korea-africa/index.html
[12] Ibid. CNN, 2017; "Idara ya Fedha inalenga watu na kampuni za Urusi na Uchina zinazosaidia serikali ya Korea Kaskazini," Kituo cha Uanahabari cha Idara ya Fedha nchini Marekani, 22 Agosti 2017. https://www.treasury.gov/press-center/press-releases/Pages/sm0148.aspx

[13] "Baraza la Usalama Linatilia Mkazo Vikwazo Dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea, na Kuidhinisha Bila Pingamizi Azimio la 2371 (2017)," *Matoleo ya wanahabari na Kuangazia mikutano ya Umoja wa Mataifa*, 5 Agosti 2017. https://www.un.org/press/en/2017/sc12945.doc.htm
[14] Ripoti ya mwisho ya Jopo la Wataalamu iliyowasilishwa kwa kutii azimio la 2094 (2013), S/2014/147 (6 Machi 2014) http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2014/147 Ukurasa: 119
[15] Ibid. p. 121
[16] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Hati ya S/2018/171. "Ripoti ya mwisho ya Jopo la Wataalamu iliyowasilishwa kwa kutii Azimio la 2345 (2017)." 5 Machi 2018. http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2018/171/Corr.1, paragrafu ya 116
[16] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 116
[17] Idara Zinazomilikiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Kongamano la Baraza la Usalama Lililoundwa kwa Kutii Azimio la 1718 (2006), Muhtasari za Kisimulizi za Sababu za Kuorodhesha, "Benki ya East Land," 29 Oktoba 2014. https://www.un.org/sc/suborg/en/sanctions/1718/materials/summaries/entity/bank-of-east-land
[18] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Hati ya S/2017/150 "Ripoti ya Jopo la Wataalamu lililoundwa kwa kutii azimio la 1874 (2009)." 27 Februari 2017. http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2017/150, table 9
[19] Idara Zinazomilikiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Orodha Iliyojumuishwa ya Vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. https://scsanctions.un.org/consolidated/#alqaedaent
[20] Idara Zinazomilikiwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Kongamano la Baraza la Usalama Lililoundwa kwa Kutii Azimio la 1718 (2006) "Kampuni ya Usimamizi ya Ocean Maritime, Ltd. (OMM)," 29 Oktoba 2014. https://www.un.org/sc/suborg/en/sanctions/1718/materials/summaries/entity/ocean-maritime-management-company%2C-limited-%28omm%29
[21] Ripoti ya Jopo la Wataalamu la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lililoundwa kwa kutii azimio la 1874 (2009), 23 Februari 2015, http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2015/131, paragrafu ya 131
[22] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Hati ya S/2016/157. "Ripoti ya Jopo la Wataalamu lililoundwa kwa kutii azimio la 1874 (2009)." 24 Februari 2016. http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2016/157, paragrafu ya 101.
[23] Ibid. S/2017/150, paragrafu za 103-104 na Nyongeza ya 70.
[24] Ibid. S/2017/150, paragafu za 110-112
[25] Ibid. S/2017/742, paragrafu ya 50
[26] Ibid. S/2017/742, paragrafu ya 29.
[27] Ibid. S/2018/171, paragrafu ya 142
[28] Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. "Azimio la 2321 (2016). Liliidhinishwa na Baraza la Usalama kwenye mkutano wake wa 7821, mnamo 30 Novemba 2016." http://undocs.org/S/RES/2321(2016), Nyongeza ya Kwanza
[29] Ibid. S/2018/171, paragrafu ya 122
[30] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 106
[31] Declan Walsh "Unahitaji Kombora la Korea Kaskazini? Pigia simu Ubalozi ulioko Kairo." Gazeti la *The New York Times*, Machi 3, 2018. https://www.nytimes.com/2018/03/03/world/middleeast/egypt-north-korea-sanctions-arms-dealing.html, na ibid. S/2017/150, Jedwali la 3.
[32] Andrea Berger amenukuliwa kwenye "Trump "anaonya" Sudani (na dunia) kuhusu Korea Kaskazini" *Arms Control Wonk*, Julai 12, 2017. https://www.armscontrolwonk.com/archive/1203587/trump-puts-sudan-and-the-world-on-notice-over-dprk/
[33] Ibid. S/2018/171, paragrafu ya 85
[34] Ibid. S/2017/742, paragrafu ya 23
[35] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 175
[36] Ibid. S/2016/157, paragrafu ya 108
[37] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 182
[38] Ibid. S/2016/157, paragrafu ya 94
[39] Ibid. S/2018/171, paragrafu ya 96
[40] Ibid. S/2018/171, paragrafu ya 144
[41] Ibid. S/2017/171, paragrafu ya 164 na nyongeza ya 43
[42] Ibid. S/2018/171, paragrafu ya 162

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com

[43] Ibid. S/2015/131. paragrafu ya 155
[44] Ibid. 1718 Orodha ya Vikwazo
[45] Ibid. S/2017/150, Jedwali la 10.
[46] Ibid. S/2017/150, paragrafu za 167, 172, 173
[47] Ibid. Walsh, New York Times.
[48] Ibid. Walsh, New York Times.
[49] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 25
[50] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 207
[51] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 208
[52] Ibid S/2017/150, majedwali ya 10 na 11
[53] Ibid. S/2017/150, jedwali la 8
[54] Tazama, kwa mfano, kutolingana baina ya nambari za pasipoti za Afisa wa Wizara ya Usalama wa Nchi ya Korea Kaskzini, Ri Won Ho, kama zilivyoorodheshwa kwenye Orodha Iliyojumuishwa ya Vikwazo na kwenye Ripoti ya S/2017/150. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. https://scsanctions.un.org/en/?keywords=&per-page=2500&sections=s&sections=s&sort=id&includes=&excludes=&committee=&nationality=&reference_from=&reference_to=. Ibid. S/2017/150, Jedwali la 8.
[55] Ibid. S/2018/171, paragrafu ya 161
[56] Ibid. S/2017/742, paragrafu ya 57
[57] Gazeti la AlYoum AlJaded: (Balozi wa Korea Kaskazini mjini Kairo anaweza kuondolewa kwa ajili ya usafirishaji haramu wa silaha) 22 Machi, 2016.
http://www.elyomnew.com/news/worldwide/2016/03/22/48128#.WwG40UiFPIU
[58] Ibid. S/2017/150, paragrafu ya 163
[59] Ibid. S/2015/131, paragrafu ya 128 na 129
[60] Donia Alwatan, https://www.alwatanvoice.com/arabic/news/2016/01/18/852255.html. 18 Januari 2016.
[61] Ibid. S/2016/157, Jedwali la 8 na paragrafu ya 175.
[62] Ibid. S/2018/171, Kiongezo cha 43
[63] Ibid. S/2016/157, paragrafu ya 108

Enrico Carisch
Simu: (610) 390 9541
Rico.carisch@comcapint.com

www.comcapint.com
110 West 94 Street 2-D
New York, NY 10025

Loraine Rickard-Martin
Simu: (917) 715 2142
loraine.rickard-martin@comcapint.com